TANGAZO LA SERIKALI NA. 249 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA BABAYU YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Babayu ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

*Tangazo la Serikali Na. 249 (Linaendelea.)*

______

JEDWALI

______

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BY1 yenye majira – nukta 795402.503MS, 9383995.191KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa MS88$^{0}$52’24.06’’MS kwa umbali wa kilomita 5.64 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BY2 yenye majira – nukta 801085.510MS, 9384106.954KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS9$^{0}$58’22.45’’ kwa umbali wa kilomita 7.45 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BY3 yenye majira - nukta 799793.143MS, 9376768.661KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa kukatiza barabara ya Dodoma - Babayu katika uelekeo wa KS78$^{0}$42’05.92’’MG kwa umbali wa kilomita 13.97 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BY4 yenye majira – nukta 786093.954MS, 9374031.301KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ23$^{0}$51’17.45’’MG kwa umbali wa kilomita 8.96 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BY5 yenye majira – nukta 789721.189MS, 9382234.068KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KS65$^{0}$44’59.47’’MS kwa umbali wa kilomita 2.96 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BY6 yenye majira – nukta 792422.141MS, 9381017.370MG; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ45$^{0}$01’27.93’’MG kwa umbali wa kilomita 4.21 hadi ulipoanzia.”

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*